BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi mungu Mtukufu, mwenye kustahiki kushukuriwa na Viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuipitia na kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuichangia kwa umakini bajeti hii kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa juhudi wanazozichukua za kuwawakilisha wananchi wao, juhudi zao zimewawezesha Wananchi kujenga imani kubwa kwa Baraza Lako. Nasi tunawaahidi kwamba tutaendelea kuwatumikia kwa dhati kama

ambavyo walivyotuamini kutuchagua na kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**
Nichukuwe fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi hii kwa umahiri na uadilifu wa hali ya juu pamoja na jitihada anazochukua za kuendeleza Uchumi wa nchi yetu kupitia sekta mbalimbali. Ni imani yetu kuwa uongozi wake bora utaimarisha miundombinu yote muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Shukrani za dhati tunazielekeza kwa Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kushauriana vyema na Mheshimiwa Rais kwenye masuala mbali mbali ya uendeshaji wa nchi yetu kwa hekima na busara ya hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**
Tunatoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa uongozi wao imara ambao umewafanya Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuanzia Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na watendaji wao wote kuwa na mashirikiano mazuri yaliyoiwezesha Kamati ya Uchumi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kuwa, mashirikiano baina yetu yatazidi kuimarika siku hadi siku na kuleta wepesi wa kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na mipango kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kubwa ya kuipitia kwa kina Bajeti ya Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mafungu yake yote (F01 hadi (F06) na kufanya marekebisho madogo madogo. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Sabiha Filfil Thani | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Hassan Hamad Omar | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Panya Ali Abdalla | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir | - Mjumbe |
| 7. Ndugu Nouman Thabit Nouman | - Katibu |
| 8. Ndugu Asma Ali Kassim | -Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Mapato ya OR-Fedha na Mipango yamejumuisha mapato ya kodi ambayo yanakusanywa na Taasisi zetu kuu za ukusanyaji wa mapato nchini ambazo ni Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania

(TRA). Kwa furaha kubwa, Kamati ilipokea taarifa ya kupanda kwa makusanyo hayo katika kipindi cha Julai – Machi, 2023 ambapo ZRA ilikusanya shilingi bilioni 449.283 sawa na asilimia 97.56 ya makadirio ya kukusanya bilioni 460.499. Makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 63.50 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2021/2022 yaliyokua bilioni 274.799

Aidha, kwa kipindi hicho Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar imekusanya jumla ya shilingi bilioni 325.611sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 337.048 ikiwa ni ongezeko la asilimia 27% ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2021/2022 yaliyokua shilingi bilioni 256.921. Tunazipongeza Taasisi hizi kwa hatua hii iliyofikiwa ambayo inatokana juhudi za watendaji na uimarishaji wa mifumo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Uchumi kwa Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

**Fungu F01 - (OR-Fedha na Mipango).**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F01 linakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania trilioni 1,945,783,279,000 na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 388,773,205,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi. Hivyo, Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi inaishauri Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kukusanya na kutumia fedha hizo kwa uadilifu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Mapato ya Idara ya Uhamiaji yaliyopo chini ya kifungu F0126 yanakadiriw kuongezeka hadi kufikia shilingi za Kitanzania bilioni 75,000,000,000 kwa mwaka 2023/2024. Kamati iliarifiwa kuwa mapato hayo yametokana na ongezeko la makusanyo ya shughuli za uhamiaji yakiwemo Ada ya usajili wa Uraia, Ada ya hati ya dharura ya kusafiria na Ada ya kibali cha ukaazi daraja A. Tunaipongeza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Uhamiaji kwa kuongeza mapato hayo ambayo yatachangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

PROGRAMU KUU YA BAJETI NA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 126,703,684,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake, ikiwa ni mapungufu ya asilimia 83.4% ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati yangu ilihoji juu ya sababu zilizopelekea kushuka kwa makadirio hayo na kuarifiwa kuwa ni kunatokana na kutimia kwa azma ya Serikali ya kupandisha mishahara ya watendaji kwa mujibu wa daraja zao kwa mwaka 2022/2023 na hivyo kutokuwa na haja ya kutenga fungu kubwa kwa ajili hiyo kwa mwaka 2023/2024. Hata hivyo, tunaishauri Wizara kuiingizia fedha kwa kiwango kikubwa Programu hii ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kushuka kwa programu ndogo ya Kusimamia Sera za Kodi na Fedha (SF010105) kutoka shilingi bilioni 51,756,186,000 mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 37,891,415,000 kwa mwaka 2023/2024 ni jambo lililoitia shaka Kamati ya Uchumi na kuhoji juu ya uwezekano wa kutimia kwa malengo ya programu ndogo hiyo na kuarifiwa kuwa, mapungufu ya makadirio hayo yanatokana na kupungua kwa ruzuku zitakazotolewa kwa Taasisi mbali mbali kama Mfuko wa barabara (ZRF) ambao utapatiwa jumla ya shilingi bilioni 15,644,300,000 na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ambayo itapatiwa shilingi bilioni 21,328,000,000.

Hivyo, Kamati inaziomba Taasisi hizo kuendelea kufanya kazi kwa bidii

kwani upunguzwaji wa ruzuku hiyo unatokana na tathmini iliyofanywa na Serikali iliyoonesha kuwa Taasisi hizo zinaweza kujiendesha kwa kiasi hicho cha fedha walichokadiriwa.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**

Usimamizi imara wa Mali za Umma na ununuzi ni chachu ya maendeleo ya nchi yetu kutokana na ukweli kwamba eneo hili ndilo linalosababisha upotevu wa mali za Serikali kwa kiasi kikubwa. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 80,416,018,000 ikiwa ni mapungufu ya asilimia 26.6% ya makadirio ya mwaka uliopita.

Kamati ilihoji juu ya upungufu huo na kuarifiwa kuwa umetokana na kushuka kwa makadirio ya fedha za ujenzi wa mji wa Serikali kutoka shilingi bilioni 92 hadi shilingi bilioni 74.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi iliarifiwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 6.618 zilipatikana katika kipindi cha Julai-Machi 2023 ikiwa ni gawio kutoka mashirika ya umma ambapo Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) lilichangia shilingi milioni 404.467, Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) lilichangia shilingi bilioni 1.5, Shirika la Bandari shilingi milioni 500, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) shilingi bilioni 3.414 na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) shilingi milioni 800. Tunatoa pongezi za dhati kwa mashirika hayo na tunayaomba yaendelee na juhudi katika utendaji wa shughuli zake ili kutoa

huduma bora kwa jamii na kutoa gawio kubwa zaidi kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu.

**Fungu F02 - Mfuko Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F02 linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 258,449,400,000 na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Tunashauri matumizi ya mfuko huu yafanywe kwa kuzingatia kanuni na sheria za nchi yetu kwa maslahi ya Taifa hili.

**Fungu F03 - Tume ya Mipango**

**Mheshimiwa Spika,**

Ni ukweli usiopingika kwamba Tume ya Mipango ni chombo muhimu cha kutoa dira ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu kupitia mipango ya maendeleo ambayo ikitekelezwa ipasavyo tutaweza kujikwamua na umasikini. Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F03 Tume ya Mipango linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 11,167,009,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Ingawa tuliarifiwa mapungufu ya fedha za matumizi ya kawaida kwa Taasisi za Serikali, bado Kamati inasisitiza kuwa fedha hizo ni chache kulingana na umuhimu wa chombo hiki kwa Taifa letu na tunaiomba Serikali kuiangalia Tume ya Mipango kwa jicho la pekee kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitishwa na kitendo cha kuipitisha Bajeti ya Tume ya Mipango na kisha uingizwaji wa fedha kuwa usioridhisha. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya shilingi bilioni 18,937,176,000 ziliidhinishwa ambapo ni shilingi bilioni 3,770,820,265.78 tu ndizo zilizoingizwa kwa ajili ya matumizi ambazo ni sawa na asilimia 19.87%. Ni jambo la kujiuliza iwapo tunakusudia kweli kupangwa na kutekelezwa mipango ya Kitaifa kwa fedha hizi zilizoingizwa? Tunaiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha changamoto hii haijitokezi tena kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**

Uratibu wa uandaaji wa feasibility study kwa miradi yote ya Serikali hufanywa na Tume ya Mipango ambapo kutokana na uhaba wa fedha, feasibility study zinashindwa kufanyika na kuendelea kuwa ni kilio kwa miradi mingi kukosa wafadhili na washirika wa Maendeleo wa kuitekeleza na hivyo Taasisi za umma kubakia na maandiko ya miradi ambayo utekelezaji wake haujulikani ni lini utafanyika.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri Wakurugenzi Mipango wa Taasisi za umma waanze maandalizi ya feasibility study za miradi ya Taasisi zao badala ya kusubiri fedha zote za shughuli hiyo.

## PROGRAMU YA KURATIBU MIPANGO YA KITAIFA NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

**Mheshimiwa Spika,**

Huduma ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini (SF030101) inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 4,419,157,000 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kiasi hiki ni mapungufu makubwa ya fedha zilizoidhinishwa mwaka 2022/2023 ambazo ni jumla ya shilingi bilioni 12,872,157,000.

Aidha, Kamati imebaini kuwa programu ndogo hii ni miongoni mwa zile zinazoingiziwa fedha hafifu mno. Hivyo, tunaiomba Serikali kuipatia programu hii fedha zote zitakazoidhinishiwa na Baraza hili ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Fungu F04 - Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali**

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F04 linalosimamiwa na Mtakwimu mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania milioni 120,000,000 na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 8,266,460,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake za msingi. Tunashauri ofisi hii ipatiwe fedha zitakazoidhinishwa na Baraza hili kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu iliyojipangia.

## PROGRAMU YA KUENDELEZA NA KURATIBU TAKWIMU RASMI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ya Uchumi imebaini kuwa matumizi ya programu ya kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii (PF0401) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imeshuka kutoka shilingi bilioni 12,772,361,000 hadi shilingi bilioni 5,975,822,000 na kuhoji juu ya sababu za kushuka huko ambapo iliarifiwa kuwa upungufu huo umetokana na kukamilika kwa mradi wa kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu chini ya ufadhili wa UNICEF. Hivyo, Kamati inaipongeza Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha mradi huo na inashauri matumizi bora ya mfumo huo kwa maslahi ya Taifa letu.

## Fungu F05 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F05 linalosimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 821,935,973,000 na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 11,142,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi. Makadirio hayo ya matumizi ni ongezeko la jumla ya shilingi bilioni 3,656,100,000 kutokana na matumizi ya mwaka wa fedha uliopita ambao uliidhinishiwa jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 7,485,900,000. Hivyo, Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kulipangia fungu hili

nyongeza ya fedha ambazo zitasaidia katika utekelezaji bora wa majukumu yake, yakiwemo yale ya usimamizi wa hazina ambayo ni chachu ya maendeleo yetu.

**Fungu F06 - Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,**

Ukaguzi wa ndani wa hesabu ni suala la msingi sana katika utekelezaji wa dhana nzima ya utawala bora. Jukumu hilo kwa hapa Zanzibar linasimamiwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu F06 linalosimamiwa na Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Serikali linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 5,081,900,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kuendelea na zoezi la uandaaji wa Mswada wa Sheria ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali ambao unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024. Tunaiomba Wizara kukamilisha uandaaji wa sheria hiyo kwa wakati uliopangwa na Serikali kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria hiyo mara baada ya kupitishwa na Baraza hili ili tuimarishe nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma na kuongeza uwajibikaji kwa viongozi wa Taasisi za Serikali pamoja na watendaji wao.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI WA UKAGUZI WA NDANI SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini (PF0601) inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi milioni 210,617,000 kwa mwaka 2023/2024. Kamati ya uchumi imesikitishwa na kiwango hiki kidogo cha fedha ambazo zinatarajiwa kutekeleza majukumu yale yale ya mwaka wa fedha uliopita ambao uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1,138,474,000. Ni dhahiri kuwa, programu hii itaathirika kiutendaji kutokana na ufinyu wa bajeti na hivyo tunaiomba Wizara kulifikiria suala hilo na kuongeza fungu la programu hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu F01 Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu F03 Tume ya Mipango, Fungu F04 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu F06 Afisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watowe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waipitishe bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………,

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kudumu ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**